**SEHEMU YA E: MASWALI YA MUKTADHA**

## KIDAGAA KIMEMWOZEA.

1. "Amani hakuwa tena na udhuru wa kutocheza na dadake...kutingisha kibiriti tena; aone kama ndani mna njiti." (uk 162)

(i) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(ii) Eleza kwa ufupi umumhimu wa Amani riwayani (alama 6)

(iii) Fafanua jinsi maudhui ya ndoa yalivyofafanuliwa riwayani. (alama 10)

2. " Katika hadithi yako usiniweke pembeni kama tanbihi, mimi na wake wenzangu..." (uk 161)

(i) Eleza kinachojiri katika dondoo. (alama 4)

(ii) Ni mbinu zipi za lugha zimetumika katika dondoo. (alama 4)

(iii) Fafanua jinsi maudhui ya ubabedume (taasubi za kiume) yamejitokeza riwayani. (alama 12)

3. "Sitaki kuishi kama kwamba sitadiriki kufa, au kufa kama kwamba sikudiriki kuishi." (uk 4)

(i) Andika muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Hukumu nihuku duniani, mbinguni ni malipo. Fafanua kauli hii kwa kurejelea riwaya. (alama 8)

(iii) Dondoa hoja nane kuhusu maudhui ya tanzia riwayani. (alama 8)

4. "kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili."

(uk 158)

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(ii) Fafanua ukweli wa dondoo kwa kutoa hoja (alama 4)

(iii) Fafanua kuhusu maudhui ya ukatili riwayani (alama 12)

5. “Matumaini yaliyopindukia ndiyo huwalewesha watu... Nasema tena tahadhari na ulevi wa ushindi.” (uk 157)

(i) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(ii) Mapinduzi/ukombozi ni jambo la muda mrefu. Fafanua (alama 8)

(iii) Mapinduzi mengi katika nchi zinazoendelea hukumbwa na matatizo waliyokuwa wakipigania. Jadili. (alama 8)

6. “Wakazi wa sokomoko wakafika kumlaki dikteta mpya aliyechukua mahali pa yule aliyetokomea” (uk 156)

(i) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(ii) Nani amekuwa kaimu mtemi. Kwa nini? (alama 4)

(iii) Dondoo hili lina taharuki mzomzo. Eleza. (alama 12)

7. Alimpigania vita malkia wa uingereza. Ni nini alichopewa ila wehu na ukata? (uk 156)

(i) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(ii) Toa sifa/tabia sita za anayezungumziwa (alama 4)

(iii) Mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda. Tetea dai hilo kwa kurejelea sampuli sampuli riwayani. (alama 10)

8. “Yaani ardhi ndicho kichocheo kikubwa cha unyama wa binadamu, ukosefu wa utu. Na madamu watu bado wanapigana.’’

(i) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(ii) Ardhi haijagawa kwa usawa riwayani. Jadili (alama 8)

(iii) Fafanua kuhusu unyakuzi wa ardhi riwayani. (alama 8)

9. “...kuwakusanya mashahidi ili kuifanya utetezi wa yusufu kuwa dhabiti katika nchi ambayo haki mahakamani ni mchezo wa bahati nasibu.” (uk 153)

(i) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(ii) Kulingana na Amani, Yusufu hana hatia. Elza (alama 4)

(iii) Uamuzi wa mahakama nchini Tomoko hufuata upepo wa viongozi. Jadili (alama 10)

10. “Jema nitakalo kulitenda silitendi; baya nisilotaka kutenda ndilo n’tendalo.” (uk 150)

(i) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(ii) Eleza masaibu manane msemaji aliyoyafanyia wenzake (alama 16)

11. “Nataka ukumbuke tu kwamba hali yangu karibu sawa na ile ya yusufu na mke wake Potifa. Ningewezaje kukutenda unyama huo...” (uk 147)

(i) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(ii) Eleza mbinu za lugha zilizotumika dondooni (alama 4)

(iii) Elza sadfa zingine sita zilipo riwayani. (alama 12)

12. “Sitalipa leo... wasikia Bwana Nasaba mbaya mbovu? Lakini nitarudi tena siku nyingine.” (uk 146)

(a) Andika muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Kuchukua sheria mikononi ni hatari kwa haki. Tetea kauli hii kwa kurejelea visa vinne riwayani. (alama 8)

(c) Jina Nasaba mbaya mbovu linamfaa mtemi zaidi. Jadili (alama 8)

13. "...Ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi inayowafanya wazalendo kulia Kidagaa kimetuozea..." (uk 140)

(a) Andika muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Matarajio ya uhuru yameponzwa na usaliti wa viongozi.jadili (alama 8)

(c) Eleza kwa utondoti wahusika wanane ambao kidagaa chao kimewaozea riwayani (alama 8)

14. "Amani hawezi kutenda kitendo kama hicho cha kurusha ndege yake kwenye anga ya mwenyewe." (uk 135)

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Amani si mfasiki kama anavyosingiziwa. Tetea dai hili. (alama 8)

(c) Fafanua sifa/tabia nane za mnenaji/mzungumzaji (alama 8)

15. "Lao kubwa lilikuwa azma ya kuibadilisha dunia yao, dunia iliyokanyanga chechele, waibadilishe kwa vyovyote viwavyo..." (uk 130)

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Kwa kurejelea visa vingine vinane elezea jinsi mbinu rejeshi imetumika riwayani. (alama 16)

16. "Agizo hilo lilimkumbusha Amani mhusika mzee kazikwisha katika riwaya iitwayo siku Njema... (uk 129)

(a) Andika muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Kwa kurejelea visa vingine vinane elezea jinsi mbinu rejeshi imetumika riwayani. (alama 16)

17. "Waandishi wazuri si lazima wawe wasemaji wazuri ... mgeni wetu hataendelea zaidi ya hapo." (uk 126)

(a) Iweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(b) Jadili kinaya kilichopo katika dondoo hili (alama 8)

(c) Fafanua sifa/tabia nane za mzungumziwa (alama 8)

18. " Kijasho chembamba kikaanza kumtoka karatasi zile zilitota pale zilipokutana na vyanda vyake!" (uk 122)

(a) Eleza muktadha wa maeneno haya (alama 4)

(b) Fafanua jinsi mbinu ya ucheshi imetumika katika matukio ya muktadha huu (alama 4)

(c) Kwa nini anayerejelewa ana sifa sufuf (alama 8)

19. " Ulevi wa ushindi ni ulevi mbaya zaidi kuliko ulevi wowote mwingine."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Ni mbinu zipi za lugha zimetumiwa dondooni (alama 4)

(c) Ulevi ni wa aina nyingi. Jadili (alama 12)

20. "...historia vilevile imeonyesha...mapinduzi...ni kubadili viongozi madhalimu kwa madhalimu." (uk 119)

(a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(b) Jadili mambo manane yanayofumba macho wanamapinduzi katika mataifa mengi yanayoendelea. (alama 16)

21. "...nchi hii hahitaji shahada za vyuo vikuu...inahitaji shahada kutoka vyuo vya maisha..." (uk 117)

(a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

(b) Eleza kwa utondoti kuhusu maudhui ya elimu riwayani (alam 16)

22. “ Viongozi wa baada ya uhuru ni wasaliti wakubwa waliorithi tabia mbaya ya mkoloni mkongwe.” (uk 115)

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Linganisha na ulinganue ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo katika Kidagaa Kimemwozea. (alama 16)

23. “ Ubwete ni ugonjwa mmoja mbaya walioambukizwa madaktari na wauguzi wengi Tomoko.” (uk 112)

(a) Andika muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Fafanua hali ya matabibu jinsi ilivyo katika nchi ya Tomoko. (alam 16)

24. “ Na ni watu wangap ihapa sokomoko uliowaadhibu kwa kutowachanja mbwa wao?...” (uk 104)